**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**WAKALA WA TAIFA WA HIFADHI YA CHAKULA**



# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KUONGEZA UWEZO WA KUHIFADHI NAFAKA

**APRILI, 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Kilimo kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, inatekeleza Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Uhifadhi wa Wakala kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka nchini Poland wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 55. Mradi huu ni wa kujenga vihenge vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 na maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000.

## 2.0 TAARIFA MUHIMU ZA MRADI

Zifuatazo ni taarifa muhimu kuhusu Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka;

**Jedwali Na. 1:** Taarifa za Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka

| | |
|---|---|
| **Jina la Mradi:** | Mradi wa kuongeza Uwezo wa Hifadhi Nafaka (Storage Capacity Expansion Project) |
| **Kiasi cha Mkopo:** | Dola za Marekani 55,000,000.00 |
| **Mchango wa Serikali:** | **USD milioni 12.84.**<br>**i. Msamaha wa VAT: USD milioni 9.9**<br>**ii. Gharama za usimamizi: USD milioni 2.94** |
| **Namba ya Mradi:** | **4497** |
| **Mtekelezaji:** | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) |
| **Msimamizi:** | Wakala wa Majengo Tanzania (Tanzania Buildings Agency –TBA) |
| **Wakandarasi:** | **i.** Feerum SA (Dodoma, Shinyanga, Makambako, Mbozi na Songea)<br>**ii.** Unia Sp.zo.o (Babati, Mpanda na Sumbawanga) |
| **Aina ya Mkataba:** | Usanifu na Ujenzi (Design & Build Contract) |
| **Gharama ya Mkataba:** | Dola za Kimarekani 53,421,697.81 |

Mradi huu ukikamilika utaongeza uwezo wa uhifadhi wa nafaka wa Wakala kutoka tani 251,000 hadi kufikia tani 501,000.

**Jedwali Na. 2:** Uwezo wa Kuhifadhi Nafaka Baada ya Kukamilika kwa Mradi

| Na. | Kanda | Uwezo wa Hifadhi kwa Sasa (Tani) | Uwezo wa Hifadhi Baada ya Mradi Kukamilika (Tani) | Mikoa ya Tanzania Bara |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Kipawa** | 52,000 | 52,000 | Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Mtwara na Lindi |
| 2 | **Arusha** | 39,000 | 79,000 | Arusha, Kilimanjaro na Manyara |
| 3 | **Dodoma** | 39,000 | 59,000 | Dodoma na Singida |
| 4 | **Makambako** | 22,000 | 62,000 | Iringa na Njombe |
| 5 | **Songwe** | 17,000 | 37,000 | Mbeya na Songwe |
| 6 | **Sumbawanga** | 38,500 | 83,500 | Rukwa na Katavi |
| 7 | **Songea** | 29,000 | 84,000 | Ruvuma |
| 8 | **Shinyanga** | 14,500 | 44,500 | Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mara, Kagera, Geita, Simiyu na Kigoma |
| **Jumla** | | **251,000** | **501,000** | |

## 3.0 NJIA YA UTEKELEZAJI WA MKATABA

Mkataba huu ni wa aina ya usanifu na ujenzi (Design and Build Contract), ambapo mkandarasi hufanya usanifu na kisha kuanza ujenzi baada ya usanifu kupitishwa na Meneja wa Mradi.

- Ujenzi wa maabara, ununuzi na usimikaji wa vifaa vya maabara;
- Ujenzi wa barabara za ndani;
- Usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na usalama (CCTV);
- Ununuzi wa vitendea kazi mfano; matrekta na elevators;
- Mafunzo ya namna ya uendeshaji wa vihenge.

## 4.0 MAENDELEO YA UTEKELEZAJI HADI KUFIKIA APRILI, 2021

Kwa sasa, mradi umefikia **asilimia 81.60%** ya utekelezaji, ambapo ujenzi wa vihenge umefikia **asilimia 88.46%** na ujenzi wa maghala na miundombinu mingine

umefikia asilimia **65.60%.** Mradi unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2021/2022.

## 5.0 KAZI ZINAZOTEKELEZWA KWENYE MRADI

Kwa sasa Wakala unaendelea na utekelezaji wa kazi zifuatazo;

- Ujenzi wa vihenge vya kisasa (silo complex) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 190,000 za nafaka;
- Ujenzi wa maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 60,000 za nafaka;
- Ujenzi wa stoo ya kuhifadhia viuatilifu na vifaa mbalimbali;
- Ujenzi wa majengo ya ofisi, sehemu ya kulia chakula (Canteen) na maliwato;

## 6.0 FAIDA ZA MRADI

Kukamilika kwa Mradi huu kunatarajiwa kuleta faida zifuatazo kwa Wakala:

1. Kuongeza uwezo wa uhifadhi;
2. Kuboresha matumizi ya technoojia ya kisasa;
3. Kuwa na uhakika wa ubora na usalama wa chakula kwa kuweza kuhifadhi nafaka kwa muda mrefu zaidi bila kuharibika;
4. Kusaidia kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno ( postharvest loss);
5. Kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato vya Wakala kupitia ongezeko la akiba ya chakula itayoweza kuuzwa/kuzungushwa kibiashara na utoaji huduma za ukaushaji, usafishaji na uhifadhi kibiashara.

## PICHA ZA MAENDELEO YA MRADI

**KANDA YA DODOMA**



**Picha Na. 1: JENGO LA KANTINI, Dodoma**



**Picha Na. 2: STOO YA MADAWA, VIFAA NA VYOO, Dodoma**


**Picha Na.3: VIHENGE VYA KISASA, Dodoma**

**KANDA YA SHINYANGA**



**Picha 4: VIHENGE VYA KISASA, Shinyanga**



**Picha Na. 5: GHALA LA TANI 10,000, Shinyanga**



**Picha Na. 6: JENGO LA UTAWALA, Shinyanga**

**KANDA YA SONGEA**



**Picha Na. 7: VIHENGE VYA KISASA, Songea**



**Picha Na. 8: GHALA LA TANI 10,000, Songea**



**Picha Na. 9: JENGO LA UTAWALA, Songea**

**KANDA YA MAKAMBAKO**



**Picha na. 10: GHALA LA TANI 10,000, Makambako**



**Picha Na. 11: VIHENGE VYA KISASA, Makambako**



**Picha Na. 12: JENGO LA KANTINI, Makambako**

## KANDA YA MBOZI



**Picha NA. 13: VIHENGE VYA KISASA, Mbozi**



**Picha Na. 14: VIHENGE VYA KISASA, Mbozi**



**Picha Na. 15: JENGO LA STOO YA VIFAA NA VIATILIFU, Mbozi**

**KANDA YA SUMBAWANGA**




**Picha Na. 16: VIHENGE VYA KISASA, Sumbawanga**



**Picha Na. 17: DRYER, Sumbawanga**



**Picha Na. 18: BLOWER SYSTEM, Sumbawanga**







**Picha Na. 19: GHALA LA TANI 5,000, Sumbawanga**




**Picha Na. 20: UTAWALA NA MAJENGO MENGINE, Sumbawanga**

**MPANDA**



**Picha Na 21: VIHENGE VYA KISASA, STOO YA MADAWA, KANTINI, Mpanda**



**Picha NA. 22: VIHENGE VYA KISASA, Mpanda**



**Picha Na. 23: VIHENGE VYA KISASA, Mpanda**




**Picha Na. 24: GHALA LA TANI 5,000, Mpanda**



**Picha Na. 25: MZANI WA KISASA, Mpanda**

**KANDA YA ARUSHA**

**BABATI**



**Picha Na. 26: VIHENGE VYA KISASA, Babati**



**Picha Na. 27: VIHENGE VYA KISASA, MAGHALA, JENGO LA UTAWALA, STOO NA KANTINI, Babati.**



**Picha Na.28: VIHENGE VYA KISASA, MAGHALA, JENGO LA UTAWALA, STOO NA KANTINI, Babati.**



**Picha Na. 29: JENGO LA UTAWALA, Babati**



**Picha Na. 30: MZANI WA KISASA, Babati**